JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: "SIASA"
Simu: 026 2322500
Email: info@orpp.go.tz
Tovuti: www.orpp.go.tz

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi
Mtaa wa Nzuguni A
P.O. Box 2851
41220-**DODOMA**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HA. 322/362/16A/22

07 Mei, 2026

Katibu Mkuu
Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)
S.L.P. 31191
**DAR-ES SALAAM**

YAH: **KUWASILISHA MAELEZO KUHUSU KUKIUKA MASHARTI YA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA KATIKA SHUGHULI ZA CHAMA CHENU**

Naomba urejee suala tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatumia fursa hii kuwataka CHADEMA kuwasilisha maelezo kuhusu utekelezaji wa masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa katika shughuli za chama chenu. Ofisi imeamua kufanya hivi kutokana na matukio kadhaa ya ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa ikiwemo yafuatayo:

3. Kwanza, katika mitandao ya kijamii kuna video inaonesha Bwana John Heche, Makamu Mwenyekiti Bara wa chama chenu akieleza kuwa, mnao mpango wa kuitisha maandamano makubwa nchi nzima ya kushinikiza Bwana Tundu Lissu aachiwe. Mitandao ya kijamii inaonesha Bwana John Heche aliongea maneno hayo tarehe 09 Aprili 2026 wakati mnaadhimisha mwaka mmoja tangu Bwana Tundu Lissu ashitakiwe kwa makosa ya jinai.

4. Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (Toleo la Urekebu la Mwaka 2023) kinaeleza kuwa, chama cha siasa kinapaswa kuendeshwa kwa kufuata Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar, Sheria ya Vyama vya Siasa …" Vilevile, kifungu cha 19(2)(f) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinaeleza kuwa, chama cha siasa hakipaswi kuruhusu viongozi au wanachama wake kutamka

au kutumia lugha za matusi, kisasi, kashfa au maneno ya uchochezi yanayoweza kusababisha au kupelekea uvunjifu wa amani au kuhatarisha usalama wa nchi." Kesi ya Tundu Lisu ipo Mahakamani, kushinikiza au kuhamasisha watu washinikize Tundu Lissu achiwe ni kuishinikiza Mahakama itoe uamuzi wa kupendelea upande fulani, suala ambalo ni kinyume cha sheria za nchi yetu. Vilevile, ni kitendo cha kuchochea watu wafanye vitendo vya ukiukwaji sheria, vinavyoweza kusababisha au kupelekea uvunjifu wa amani na kutishia usalama wa nchi yetu.

5. Pili, katika mitandao ya kijamii kuna video nyingine inaonesha mwanachama na kiongozi wa CHADEMA Bwana Oliver Kisaka, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga, akieleza yafuatayo, nanukuu *"… nyinyi watu wa kibamba mnaweza kuwa mnajichukulia poa lakini nyinyi kwenye siasa za Tanzania na siasa za Dar-es salaam, nyinyi ni watu wa kuigwa na ni watu mfano, wakati machafuko yanatokea tarehe 29 oktoba mimi ni moja ya watu ambao waliokuwa wamekamatwa na tulikuwa tumewekwa sehemu isiyojulikana, wakati mitandao inarudi internet inarudishwa mimi nilikuwa nataka kujua watu wameandama au hawajaandamana, wamepiga kura au hawajapiga kura, askari mmoja akaja na simu yake baada ya mitandao kufunguliwa, nikamuuliza bwana vipi, akasema bwana nimekuletea kitu uone jinsi watu walivyosimama, nikasema watu wa wapi, akasema hawa watu ni wa kibamba na ubungo, katika sehemu iliyoonesha msimamo wa "no reform no election" ni Kibamba na Ubungo, maana yake ni kwamba inawezekana mageuzi makubwa ya nchi hii uasisi wake ukatokea katika jimbo hili msishangae"*

6. Maneno ya mwanachama huyu yanakiuka masharti ya kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura yanayotaka chama cha siasa kuendeshwa kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar, Sheria ya Vyama vya Siasa…. Pia, masharti ya kifungu cha 19(2)(c) cha Sheria ya Vyama vya Siasa yanayokataza katiba, kanuni, sera au vitendo vya chama cha siasa kuruhusu au kushawishi matumizi ya nguvu au vurugu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa. Vilevile, masharti ya kifungu cha 19(2)(f) cha Sheria ya Vyama vya Siasa yanayokataza chama cha siasa kuruhusu viongozi au wanachama wake kutamka au kutumia lugha za matusi, kisasi, kashfa au maneno ya uchochezi yanayoweza kusababisha au kupelekea uvunjifu wa amani au kuhatarisha usalama wa nchi.

7. Tatu, tarehe 05 Mei 2026 CHADEMA mlitoa taarifa kwa umma ambayo ina maneno na maelezo ya kashfa na uchochezi yanayokiuka kifungu cha 9(2) na 19(2)(f) cha Sheria ya Vyama vya Siasa. Baadhi ya maneno hayo ni yafuatayo, nanukuu:

*"19…Samia Suluhu ambaye ni mtawala wa mabavu asiyechaguliwa na wananchi wa Tanzania."*

*"32 inaeleza kuwa, nanukuu "Kamati Kuu inasisitiza kuwa pale haki za kidemokrasia na njia zote za kujieleza na kutetea haki za mtu zinapofungwa kunasababisha watu kutokuwa na njia nyingine bali kuingia barabarani na kueleza chuki zao na kudai mabadiliko ya kweli"*

*"56… je, wananchi waende wapi pengine isipokuwa kuingia mtaani?"*

*"34. Kamati Kuu inasema kuwa kuwataka wananchi waheshimu sheria za nchi wakati huku genge la watu wachache kupitia CCM na kiongozi wao Samia Suluhu Hassan wakisigina haki zao ni kuwageuza wao kuwa ni mandondocha…Vijana na wote waliouawa mnamo tarehe 29 Oktoba 2025 na wale waliotekwa, kuteswa, na kuuawa kabla na baada ya tarehe hiyo ni Mashujaa wa taifa letu na CHADEMA inawatangaza hivyo."*

*"35… Samia Suluhu Hassan alipotimiza nia yake ya kutwaa madaraka kwa nguvu na kuapishwa huko Dodoma."*

*"41… Samia Suluhu Hassani, hata kwa madaraka ya uraisi wa wizi na haramu aliojipachika kwa mabavu, hana"*

*"37… Ni polisi, watu wa usalama, askari wa KMKM, na askari waliokuwa wakizungumza lugha ya Kiingereza chenye lafudhi ya lugha za Uganda ndio walikuwa mitaani na wanaodaiwa kufanya mauaji hayo ya kinyama."*

*"38… Samia Suluhu na chama chake cha CCM kwani wao ndio watuhumiwa nambari moja wa mauaji ya kinyama na kishetani yaliyofanywa kabla, mnamo, na baada ya tarehe 29 Oktoba 2025."*

*"39. Mara baada ya mauaji hayo na kuapishwa kwa nguvu kwa Samia Suluhu Hassan, katika kambi moja ya Jeshi Mkoani Dodoma…"*

*"47. Kamati Kuu imeamua kuwaambia Watanzania kuwa kile kilichofanywa na Samia Suluhu na genge lake linalotawala nchi yetu*

*kwa mabavu kwa kutumia Polisi na vyombo vingine vya usalama vya usalama ni batili na ukiukwaji wa wazi kabisa wa ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania."*

*"48...kuficha ukweli, kudogodesha matukio mabaya yaliyofanywa na Samia na Jeshi la Polisi na vikosi vingine vya usalama hata wanaodaiwa kuwa mamluki kutoka nje ambao walifika na kuua watu kwa maelfu na si mamia yanayotajwa na Tume hiyo haramu na batili."*

*"60... kwani Jeshi la Polisi na vyombo vya usalama wao walitekeleza amri ya kupiga risasi ili kuua (shoot to kill)"*

*61. Kamati Kuu imebaini kuwa licha ya kuwepo kwa kauli za kutoka kwa Samia Suluhu na viongozi wa CCM juu ya ushiriki wao katika kuamurisha kupigwa kwa risasi kwa waandamanaji halali wa demokrasia mnamo tarehe 29 Oktoba 2025."*

*"49...utawala wa sheria katika nchi yetu umeporomoka na kilichopo sasa ni ubabe tu"*

*"56... Je Bunge linapogeuka muhuri wa genge la watawala waovu na wababe na linaloshangilia kuibwa na kufisadiwa kwa mali na rasilimali za nchi ... Mahakama ikitoa kila aina ya kinga kwa genge hilo kuendelea kuifisadi nchi"*

*"66...Tume hiyo haramu ya Chande ilijigeuza kuwa kitengo cha propaganda cha CCM na Samia Suluhu Hassan kwani ilichokisema hakina mantiki na ni kejeli."*

*"79. Kamati Kuu inadai kurudiwa kwa uchaguzi mkuu ili Watanzania wasiendelee kutawaliwa kimabavu na wauaji ambao wametwaa madaraka kwa kutumika polisi na usalama wa taifa. Uchaguzi huo lazima usimamiwe na Tume Mpya kabisa ya Uchaguzi.Kamati Kuu inasisitiza kuwa Samia Suluhu Hassan amejiweka madarakani kama raisi wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na Serikali yake yote ni ya kibabe kwani ni Kiongozi aliyetwaa madaraka kwa mtutu wa bunduki na kwa kumwaga damu ya maelfu ya Watanzania. Si raisi wa Watanzania!"*

8. Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaruhusu Watanzania kuanzisha vyama vya siasa na kutoa maoni yao bila kukiuka sheria za nchi. Hivyo, chama cha siasa kutoa maoni kwa lugha za kashfa, dhihaka na uchochezi kama ilivyo hapo juu, ni ukiukwaji wa Katiba na sheria za nchi ambao haupaswi kuwepo, kwa sababu chama cha siasa kina uwezo wa kuwasilisha ujumbe wake bila ya kukiuka sheria.

9. Hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kifungu cha 39(2)(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kama kilivyorekebishwa na kifungu cha 19 cha Sheria Namba 3 ya Mwaka 2024 na kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha Sheria ya Vyama vya Siasa kama kilivyorekebishwa na kifungu cha 21 cha Sheria Sheria Namba Namba 3 ya Mwaka 2024, Msajili wa Vyama vya Siasa anawataka CHADEMA muwasilishe maelezo kueleza kwa nini usajili wa chama chenu usisimamishwe au chama chenu kutozwa faini kwa kukiuka masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa, ikiwemo masharti ya usajili. Maelezo yenu yawasilishwe Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa siyo zaidi ya tarehe 20 Mei 2026 saa tisa na nusu alasiri. Nimekutumia video hizo kwa njia ya barua pepe ya chama na yako binafsi na WhatsApp.

10. Wako katika ujenzi wa Taifa.

Sisty L. Nyahoza

Kny: **MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**